**World Miracle Mission Centre- Elumaka Foundation College**

**P.O.BOX 47, BUKOMBE, GEITA TANZANIA: Admission:** +255-764-397 265

**General:** +255 684 637 782**: E:** pastorjustice@gmail.com: **W:**www.worldmiraclemission.org

Kumb Na: WMMC/ EFO/AD/1/2016 TAREHE: Agosti 2016

Kwa Mzazi/Miezi wa.......................................................................................

Napenda kuchukua nafasi hii kukupa hongera kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga na Chuo cha Mafunzo ya awali ya Uuguzi Cha ELUMAKA FOUNDATION (EFOCO). Hiki ni chuo kishirikishi (Associate and Affliate) cha Huduma ya Injili na Umishonari ya World Miracle Mission Centre, yenye makao yake makuu Dar es salaam, Tanzania. Chuo hiki hutoa vyeti vya ujuzi vya elimu ya kimwili na ya kiroho. Kozi zinazofundishwa katika chuo hiki ni:

**Kozi ya Pre-Nursing; Kozi ya Kompyuta; Kozi ya Bible Studies; Kozi ya Uinjilisti; Kozi ya Kupanda Makanisa; Kozi za Utume; Kozi za umishonari; Na Kozi nyingine za Utawala, Manunuzi; Biashara na Ujenzi.**

Chuo pia kinatoa masomo kwa wanafunzi wa kodato cha Nne na Sita wanaotaka kurudia mitihani kwa masomo ya Civics, Mathematics, Geography, History, Physics, Chemistry, Biology, Book Keeping na Commerce.

Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ............... kabla ya saa 11:00 jioni bila kukosa. Endapo hatafika katika tarehe hiyo uongozi wa chuo utakuwa huru kutoa nafasi hiyo kwa mwingine aliye katika orodha ya akiba (Reserve list).

**NAMNA YA KUFIKA CHUONI:**

Chuo cha ELUMAKA kipo Mkoa wa Geita, wilaya ya Bukombe, Kata ya Lyamba Mgongo na kijiji cha Lyamba Mgongo. Ukifika stendi ya mabasi ya Ushirombo panda haisi zinazokwenda Kahama mjini, Shuka Lyamba Mgongo.Kwa wale wanaotokea Kanda ya Ziwa na Kusini na Mashariki mwa Tanzania, Panda mabasi yanyokwenda Kagera, Ushirombo. Nauli ni sh 1,000/-. Ulizia Chuo cha World Miracle Mission Centre-ELUMAKA, kiko karibu na Sleeaway Lodge.

**YAFUATAYO NI MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA AJILI YA MWANAO:**

1. **Karo ya Chuo:**

   a) Unatakiwa kulipa jumla ya shilingi **TZS. 1,510,000/-**kwa ajili ya ada kwa mwaka;

**TZS. 840,000/-** muhula wa kwanza na **TZS 670,000/-** muhula wa pili. Unatakiwa kulipa TZS **191,000/-** kwa ajili ya sare za chuo, pamoja na mahitaji mengine kama yalivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini.

| EFOCO Fee Structure | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | **Description** | **1st SEMISTER** | **2nd SEMISTER** |
| | | **TZS** | **TZS** |
| 1 | Application Fee | 40,000 | - |
| 2 | Registration fee | 40,000 | - |
| 3 | Tuition fee | 500,000 | 250,000 |
| 4 | Medical Fee | 20,000 | - |
| 5 | Caution money | 40,000 | - |
| 6 | National Health Insurance Fund | 40,000 | 40,000 |
| 7 | Hostel Fee | 10,000 | 10,000 |
| 8 | Student's identity card | 10,000 | - |
| 9 | EFOCO Examination fee | 40,000 | 40,000 |
| 10 | Graduation Fee | - | 30,000 |
| 11 | Meal Allowance fees | 100,000 | 100,000 |
| 12 | Practical Training Field Money | - | 200,000 |
| | **SEMISTER FEE PER STUDENT IN TZS** | **840,000** | **670,000** |
| | **TOTAL ANNUAL FEE PER STUDENT IN TZS** | **TZS** | **1,510,000** |

b) Fedha hizi zote zitalipwa kama ifuatavyo:

(i) Karo Zote (Fees) Kiasi cha **TZS 1,510,000.** Lipia akaunti yetu ya **WORLDMIRACLE MISSION CENTRE CRBD A/C No. 0150 222 9696 00**, katika tawi lolote la benki ya CRDB.

**(ii)** Mahitaji ya mengine kama sare yanayolipiwa yatalipiwa Chuoni Kwa Jumla ya **TZS 191,000.**

**(iii)** Kwa ajili ya kumbukumbu na ufuatiliaji hakikisha umetaja kwa mhudumu wa benki majina matatu ya mwanafunzi kisha andika nyuma ya hati ya malipo hayo majina matatu (Pay-in.-slip) na ifikishwe chuoni ili ikatiwe risiti. Endapo hutatuletea "Pay-in-slip original" hatutakuwa na udhibitisho kuwa umeshalipa benki. Fedha nyingine za matumizi ya mwanafunzi zisiingizwe katika akauntiya shule ziletwe chuoni zitunzwe na mhasibu.

**NB: ANGALIZO:**

i. Fedha ikiingizwa benki hairudishwi na wala haitaweza kuhamishiwa kwa mwanafunzi mwingine.
ii. Malipo kwa njia ya simu (M-PESA,TIGO PESA, AIRTEL MONEY

n.k) kupitia kwa mfanyakazi yeyote hairuhusiwi kabisa.

iii. Malipo ya fedha taslimu hayaruhusiwi pia kulipia karo.

## 2. Mahitaji ya kulipia Chuo

a) Sare za Chuo na mahitaji mengine

| | Mahitaji ya Kulipia | Jumla | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1 | Sketi 2 kwa wasichana au/suruari 2 kwa wavulana @ 15,000 X 2 | 30,000 | |
| 2 | Mashati 2 ya Chuo@ 8,000=1x 2 16,000/- | 16,000 | |
| 3 | Soksi pea 2 | 50,000 | |
| 4 | Nguo za kushindia (sketi 2 kwa wasichana au Suruali 2 kwa wavulana. | 30,000 | |
| 5 | T-shirt zenye nembo ya shule 2 @ 10,000/- x 2 | 25,000 | |
| 6 | Sweta 1 | 20,000 | |
| 7 | Track Suit | 20,000 | |
| | **JUMLA TZS** | **191,000** | |

b) Mahitaji mengine ambayo mwanafunzi anahitaji kuja nayo siku ya kuripoti shuleni ni;

| | Mahitaji ya Kuja Nayo Mwanachuo | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Biblia NIV | Lazima |
| 2 | Shuka 3 | Lazima |
| 3 | Chandarua | Lazima |
| 4 | Mto/Foronya yake | Hiari |
| 5 | Blanketi 1 | Hiari |
| 6 | Karatasi A4-Rim 1 | Lazima |
| 7 | Daftari 12 Kubwa ( Counter book) | Lazima |
| 8 | Ndoo ya Kuogea | Lazima |
| 9 | Kikombe/ bakuli/ Kijiko/ Sahani | Lazima |

c) Pia: Mahitaji mengine ya muhimu kama miswaki, dawa ya meno, mafuta, sabuni, kandambili n.k. yanapatikana katika maduka karibu na chuo kwa bei nzuri.

## 3. Utunzaji wa mali za shule:

Ni jukumu la kila mwanafunzi kutunza vyema mali yake binafsi na mali ya Chuo. Mwanafunzi atakayeharibu au kupoteza mali ya chuo atalipishwa kulingana na thamani ya uharibifu alioufanya.

## 4. Siku ya kutembelea wanafunzi:

Siku ya kutembelea wanafunzi ni mara moja kwa mhula, utafahamishwa siku utakayo mleta mwanafunzi shuleni.

**5. Nidhamu ya Kiroho**

Elumaka Foundation College ni Chuo ya Ki-pentekoste, na kinajali na kufundisha wanafunzi kumcha Mungu ili wawe raia wema wa nchi yetu, na viongozi wa baadaye wa serikali na Kanisa. Ni lazima kila mwanafunzi kuhudhuria ibada zinazoendeshwa kwa mujibu wa imani ya kipentekoste. Kufanya ibada zilizo kinyume na imani ya kipentekoste ni kosa na atakayekutwa anafanya hivyo atachukuliwa hatua za kinidhamu. Ni imani yetu kuwa wewe mzazi utashirikiana vyema na uongozi wa Chuo ili kufikia lengo hilo bila kumtetea mwanao anapokosea.

**6. Vitu visivyoruhusiwa:-**

(a) Ni kinyume cha taratibu zetu kwa Mzazi/Mlezi/jamaa au rafiki kuwasiliana na mwanafunzi kwa njia ya simu kupitia kwa mfanyakazi au kwa namna yoyote ile. Mawasiliano yote yapitie kwa Mkuu wa Chuo.

(b) Ni makosa kwa mwanafunzi kuwa na dawa zozote bwenini. Dawa zote zikabidhiwe kwa Matron au Patron kwa maelezo siku ya kwanza anaporipoti. Matroni wa shule atasimamia matumizi ya dawa kwa mwanafunzi.

(c) Unatakiwa ununue viatu vyeusi visivyo na soli ndefu, (kwa wasichana na Wavulana) viatu vilivyochongoka mbele visivyo na kamba hasa kwa wavulana havitakiwi.

(d) Wanafunzi wa kiume hawaruhusiwi kuwa na mikanda (belts) yenye bankoli kubwa na picha zisizoeleweka.

(e) Mwanafunzi haruhusiwi kuja *au* kuletewa <u>chakula</u> cha aina yoyote ile.

**7. Mawasiliano:**

Unaweza kutumia namba zifuatazo kuwasiliana nasi:

(a) Ofisi ya Mkuu wa Chuo .........0764- 397 265

(b) Ofisi ya Taaluma................. 0684 - 637 782

(c) Ofisi ya Mkurungenzi ...........0755- 754 924

<u>**Muhimu:**</u>

i. Fomu iliyoambatanishwa na barua hii ni ya kupima afya ya mwanao, baada ya kupimwa na daktari aliyethibitishwa, ijazwe na kupigwa muhuri wa daktari husika na kuletwa chuoni siku ya kuripoti.
ii. Chuo haitahusika na kuwasafirisha wanafunzi hivyo kila mzazi/mlezi anao wajibu wa kumleta mwanaye shuleni siku ya kufungua shule na kuja kumchukua siku ya kufunga shule.

Fuata maelekezo yote kwa usahihi ili kuepuka usumbufu.

**SHERIA NA KANUNI ZA**

**ELUMAKA FOUNDATION COLLEGE**

**MWAKA 2016/17**

SOMA KWA MAKINI.

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kufahamu na kutii amri na kanuni za Chuo kwa makini. Mwanafunzi atakayevunja sheria ama kwenda kinyume na kanuni za chuo aidha ataadhibiwa au atarudishwa nyumbani kwa mudao Mwanafunzi asiyeweza kubadili tabia yake mbovu atafukuzwa toka shuleni.

SHERIA NA KANUNI ZA CHUO

1. Ni lazima kila mwanafunzi kuhudhuria vipindi vyote na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani atakayopewa na walimu au watahini wengine (NACTE) nk.

2. Ni lazima kila mwanafunzi kuhudhuria ibada zinazoendeshwa kwa mujibu wa imani ya kipentekoste.

3. Ni lazima kila mwanafunzi awe amevaa sare ya shule wakati wa vipindi darasani na avae vazi la nyumbani anapokuwa nje ya chuo.

4. Ni lazima kila mwanafunzi kuheshimu walimu, wafanyakazi wengine wa Chuo, wazazi na viongozi wote wa World Miracle Mission Centre na serikali ya wanafunzi.

5. Wanafunzi hawaruhusiwi kuvaa kofia, malapa, kandambili, au viatu vya wazi wanapokuwa darasani au ibadani.

6. Wasichana hawaruhusiwi kuvaa bangili, shanga za shingoni au kujipamba kwa kupaka rangi au wanja midomoni, nk.

7. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila kibali cha Mkuu wa shule au Matron Ruhusa zote za kwenda mjini au nyumbani hutolewa na Mkuu wa Chuo.

8. Wanafunzi hawaruhusiwi kulia chakula nje ya Bwalo au darasani bila ruhusu ya kufanya hivyo Chakula kiliwe kwa ustaarabu.

9. Ni marufuku mwanafunzi asiyekuwa katika zamu kuingia jikoni.

10. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingia katika ofisi ya walimu, au kwenye nyumba za walimu au wafanyakazi wengine wa Chuo bila sababu maalumu.

11. Kila mwanafunzi anawajibika kutunza mali ya Chuo Ni marufuku kuweka alama, michoro au maandishi kwenye kuta za majengo, madawati, viti, meza au sehemu nyingine kwenye eneo la Chuo. Mwanafunzi yeyote atakayeharibu au kuchafua mali ya Chuo kwa kukusudia atawajibika

kulipa na anaweza kufukuzwa toka Chuo.

12. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingiza wageni Chuoni bila taarifa kwa uongozi wa chuo. Ni lazima wageni wote watambulishwe kwa Mwalimu wa Zamu au kwa Mkuu wa Chuo. Ni lazima wageni waondoke toka kwenye eneo la Chuo kabla ya saa 11:00 jioni.

13. Vitu vifuatavyo haviruhusiwi Chuoni: Ibada zilizo kinyume na Upentekoste, madawa ya kulevya, Silaha ya aina yoyote, wala kampeni za kisiasa.

14. Ulevi, kupigana, kutumia lugha mbaya (chafu), makelele, uasheratiau uzinzi, kufanya mapenzi, kuvuta sigara au bangi na madawa ya kulevya ni marufuku kabisa.

15. Mwanafunzi haruhusiwi kuchora au kuandika maandishi ya aina yoyote juu ya sehemu yoyote ya mwili wake kama mikononi, kwenye mapaja, kifuani au mgongoni kwa kutumia wino au kifaa chochote.

16. Kiingereza ni lugha ya mawasiliano kwa wanafunzi wote hapa Chuoni. Ni lazima wanafunzi wawasiliane kwa kiingereza kwa ajili ya Masomo; pia wawasiliane na walimu wao kwa kiingereza ndani ya madarasa. Kiswahili na lugha za kimakabila zitumike tu nje ya darasa.

17. Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya lbada, semina, huduma za kimishonari na maombezi.

18. Mtu atakayevunja sheria za chuo kwa kujifanya kwamba hazijui ama hazielewi hatasikilizwa, na hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa chuo..

<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<<>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>>

**MAKUBALIANO KATI VA MZAZI/MLEZI**
**NA UONGOZI WA CHUO**.

Nakusalimu katika jina la Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo.

ELUMAKA Ni chuo cha Kipentekoste ambacho kimelenga kuwalea wanafunzi katika maadili mema kiroho, kinidhamu na kitaaluma ili waweze kufikia malengo yao.

Tunaomba ahadi yako ya kushirikiana nasi katika malezi ya mwanao, na kwamba unakubaliana na sheria na taratibu zote za chuo kama zinavyooneshwa hapo nyuma.

AHADI YANGU: Mimi................................................Mzazi/mlezi wa....................................................

Ninakubali kushirikiana na chuo na kwamba mwanangu atafuata/hatafuata sheria na taratibu zote za Chuo. Na kwamba hataruhusiwa kupata cheti cha kuhitimu kama hatafikisha wastani wa alarna 50 mwisho wa kila mwaka wa masomo.

Sahihi

Namba za simu

1........................ ......................

2... .. ..........................................

3...... .......................................

Anuani ya Posta

NB: *Mwanao hatapokelewa Chuoni endapo hataleta fomu hii ikiwa imejazwa kwa usahihi na ufasaha.*

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

1. Student 's name. .. ..................... ..................... .. ..................

2. TO: Medical Officer Incharge of....... ..... ...................(Hospital)

3. Please examine him/her in respect of the hereunder listed Medical disorders/diseases

| DISORDER/DISEASE | | DOCTOR'S FINDINGS | DOCTOR'S COMMENTS | DOCTOR'S SIGNATURE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | | |
| 2 | Typhoid | | | |
| 3 | S.T.D's | | | |
| 4 | Blood Pressure | | | |
| 5 | Deafness | | | |
| 6 | Eyesight | | | |
| 7 | Eye disease(s) | | | |
| 8 | Ear disease(s) | | | |
| 9 | Epilepsy | | | |
| 10 | Pregnancy | | | |
| 11 | Blood Sugar Level | | | |
| 12 | Any Other | | | |
| 13 | Any Other | | | |

CERTIFICATE OF FITNESS

To: PRINCIPAL OF ELUMAKA FOUNDATION COLLEGE

I have subjected the above named student to a thorough medical examination and the results as shown on the table above.

Doctor's Name......... ... ................................. Signature.. ..........................